Toleo 20

# Ukweli wa Injili

*Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote*

## SIKU YA BWANA

Mtume Yohana, mtume ambaye alipendwa sana na Yesu alihamishwa na kupelekwa kisiwa cha Patmo ambako aliandika na kusema: "Nalikuwa katika Roho, siku ya Bwana; nikasikia sauti kuu nyuma yangu, kama sauti ya baragumu" (Ufunuo 1:10). Yohana huyu alipewa (kitabu cha) Ufunuo (wa Yohana) katika kipindi maalum kilichoitwa "Siku ya Bwana." Hii ilikuwa ni siku ya kwanza ya wiki, maanake Jumapili.

Siku ya Jumamosi, ambayo ilikuwa ni siku ya mwisho ya wiki ilikuwa spesheli kwa Wahayudi walioshi katika Agano la Kale. Wao walifungwa na amri hiiyo iliyowaamurisha kudumisha Sabato kama siku takatifu ya mapumziko na ya kufanya ibada. Lakini baada ya Kristo kuja ulimwenguni Wakristo hawakuwa tena chini ya sheria na hawakufungwa na matakwa yake. Ndiposa Wakristo wale wa kwanza walikuwa na tabia (mpya) ya kukutana kwa ibada katika siku ile ya kwanza ya wiki ambayo ilijulikana kama "Siku ya Bwana."


Jumapili ilikuwa na umuhimu wake kwa waumini kwa maana Bwana Yesu alifufuliwa kutoka kaburini katika siku hiyo ya kwanza ya wiki, baada ya yeye kusulubiwa. "Hata siku ya kwanza ya juma, ilipoanza kupambazuka, walikwenda kaburini . . . Wakalikuta lile jiwe limevingirishwa mbali na kaburi, wakaingia, wasiuone mwili wa Bwana Yesu" (Luka 24:1-3).

Siku ya Jumapili ilipata umuhimu mkubwa zaidi kama siku maalum kwa maana Roho Mtakatifu alimwagwa kwa waumini katika siku ya Pentekoste (Matendo 2:1-4), ambayo ilikuwa ni siku ya kwanza ya wiki. Sherehe za Pentekoste ambazo zilianzishwa ili kusherehekea kutolewa kwa Sheria ya Musa katika Mlima Sinai ni sherehe ambayo ilifanywa siku hamsini baada ya Pasaka. Kwa njia hiyo pia Kristo alisulubiwa kwa ajili ya dhambi za mwanadamu katika Siku ya Pasaka, na baadaye katika Siku ya Pentekoste (wakati ambao pia Agano la Kale lilitolewa) Roho Mtakatifu akashuka na kuandika sheria ya Mungu mioyoni mwa waumini.

Basi ni jambo ambalo linaweza kueleweka kwa urahisi ni kwa nini wafuasi wa Kristo walianza kuabudu siku ya Jumapili badala ya Jumamosi. Haikuwa lazima wao kufuata maagizo ya Sabato na siku ya kwanza ya wiki ilikuwa na maana na umuhimu zaidi kwao.

Kulingana na Maandiko kanisa hilo la kwanza lilikuwa linaabudu siku ya Jumapili: "Hata siku ya kwanza ya juma, tulipokuwa tumekutana ili kumega mkate, Paulo akawahutubu, akiazimu kusafiri siku ya pili yake, naye akafuliza maneno yake hata usiku wa manane" (Matendo 20:7). Naye Mtume Paulo alitoa wosia kwa Wakristo katika 1 Wakorintho 16:1-2 na kuwaambia, "Kwa habari ya ile changizo kwa ajili ya watakatifu, kama vile nilivyoamuru makanisa ya Galatia, nanyi fanyeni vivyo. Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake, kwa kadiri ya kufanikiwa kwake; ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja." Wao walitoa sadaka zao katika siku

*(Inaendalea kutoka ukurasa 2)*



"Jumapili nayo ilikuwa na umuhimu wake kwaa waumini kwa maana Bwana Yesu alifufuliwa kutoka kaburini katika siku hiyo ya kwanza ya wiki..."


Tahariri 3

Mwongozo wa Kujifunza Biblia: Sabato 4

Mafundisho ya Biblia Kuhusu Sabato 5

Maswali na Majibu 7

Je, Wajua?

Neno Linalofaa kwa Msimu Huu 8

# Mambo Ambayo BIBLIA Inafundisha Kuhusu...

**Neno la Mungu**

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

**Uhusiano wa Upendo**

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

**Toba**

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

**Uzao Mpya**

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6

**Uhuru Kutokana na Dhambi**

1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

**Ujazo wa Roho Mtakatifu**

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

**Utakatifu**

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16, Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

**Ufalme wa Mungu**

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

**Kanisa**

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18

**Umoja**

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

**Kanuni za Kanisa**

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27, Yn. 13:14-17

**Uponyaji wa Kiungu**

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

**Utakatifu wa Ndoa**

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, I Kor. 7:10-11

**Urembo wa Nje**

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

**Mwisho wa Nyakati**

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46

**Kupenda Amani**

Lk. 6:27-29, 18:20

**Ibada**

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

**Wajibu Mkuu**

Mk. 16:15

*(Endelea kutoka ukurasa 1)*

ya Jumapili badala ya siku (ya hapo mbeleni) ya Sabato, na pia ni dhahiri kwamba Wakristo hao walikuwa wakikutana na kuabudu katika siku ya Jumapili.

Tangu wakati wa Yesu kumekuwa na tamaduni kote ulimwenguni ya Wakristo kutenga Jumapili, yaani Siku ya Bwana kama wakati maalum wa ibada ya pamoja. Hata ingawa Maandiko hayajaamuru jambo hilo kwa njia ya moja kwa moja, kama yalivyoamuru kuhusiana na siku ya Sabato katika Agano la Kale, maandiko yenyewe yanafundisha kwamba tusiache mazoea ya kukutana pamoja (Waebrania 10:25).

Hakuna makosa Wakristo kukutana siku nyingine isipokuwa ile ya Jumapili kwa ajili ya ibada, lakini ni makosa yaliyo dhahiri kwa makusanyiko kukutana siku ya Jumamosi kwa lengo la kudumisha Sabato. Hii ni kwa sababu wao huwa wakijaribu kushika sheria ambayo imepita na hakuna utakatifu unaopatikana kutokana na kuzingatia siku hiyo. Huku wakijaribu kudumisha sheria ya kuonekana na wanadamu wao hupoteza ukweli mkuu zaidi wa uhuru na utakatifu wa kweli ambao hupatikana ndani ya Yesu Kristo.

Hata ingawa Wakristo wengine wanaweza kukutana siku ya Jumamosi ili kufuata sheria za nchi zao na kulingana na ratiba tofauti za kikazi hasa katika nchi za Kiislamu, lakini sisi wote tunaweza kupata ujuzi na urembo wa uhuru wa Siku ya Bwana katika kila siku ya wiki.

—mws

## UKWELI WA INJILI

Gazeti la '*Ukweli wa Injili'* huchapishwa kwa jina la Bwana kwa matumizi ya watu wa mataifa yote kwa kusudi la kuimarisha na kuwahimiza watu wote katika ukweli wa neno la Mungu. Gazeti hili hufundisha na kueneza ukweli wa Biblia ambao umethibitishwa tangu nyakati za Yesu Kristo na mitume.

Neno la Mungu ndio mwongozo halisi na wa kipekee wa imani. Linafundisha wokovu na ukombozi kutokana na dhambi unaoletwa na utakaso wa Yesu Kristo; ambao hufuatiwa na ujazo wa Roho Mtakatifu anayemwongoza mhudumu, kumwonyesha njia, na kumpatia nguvu; pia unamletea mtu utakatifu halisi katika kila fani ya maisha yake; na pia kuleta umoja na utangamano wa watu wa Mungu. Huduma inayokubalika na Mungu inatokana na mtu kuwa na uhusiano wa kibinafsi na wa upendo ambao msingi wake ni ukweli.

Waandishi: Michael na René Smith

## UAGIZAJI

*Ukweli wa Injili* ni gazeti la kieletroniki linalochapishwa kila robo ya mwaka kwa jinsi Mungu anavyotuongoza. Tutembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org ili uagize jalida hili kupitia kwa orodha yetu ya anwani pepe na upokee toleo lako la wakati huu. Hebu jisikie huru kutumia orodha ya majina na anwani pepe za watu wengine ambao wangependa kupokea toleo hili kutoka kwa mwandishi wa jalida la Ukweli wa Injili.

## WASILIANA NASI

Gazeti a Ukweli wa injili linachapishwa katika mataifa mbalimbali ili kusambazwa katika maeneo hayo. Kazi hii na zingine za kimishenari ambazo sisi hufanya huwezekana kupitia kwa matoleo ya kujitolea yanayotolewa kwa jina la Kanisa la Mungu.

The Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@thegospeltruth.org

# Tahariri



*Basi, imesalia raha ya sabato kwa watu wa Mungu. Kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi zake* —Waebrania 4:9-10.

Pumziko la roho ya mwanadamu ambalo hupatikana ndani ya Yesu Kristo ni lenye utukufu mkubwa. Kupitia kwa Yesu Kristo kuna amani ambayo mtu hupata ambayo kamwe haiweleki na mwanadamu. Amani hii hushinda matatizo na dhoruba za maisha na huwa imemwingia sana mtoto wa Mungu na kukuza mizizi moyoni mwake. Amani hii haitokani na bidii zetu za kibinafsi au haitokani na utakatifu wetu bali hutokana na uwepo wa Mwana wa Mungu.

Katika robo hii ya mwaka tunaendelea kujenga juu ya msingi ambao uliwekwa katika nakala ya 18 kuhusiana na agano mbili ambazo Mungu alianzisha kati yake na wanadamu. Udumishaji wa siku ya Sabato ilikuwa moja ya Amri Kumi za Mungu zinazopatikana katika Agano la Kale. Lakini hii ilikuwa moja tu ya amri kadhaa kati ya hizo kumi ambazo hazikurudiwa katika Agano Jipya. Kiini chake ilikuwa ni ufuataji wa amri kwa kufanya sherehe, na kwa njia ya kimwili, ambayo kupitia kwake kuliwekwa msingi wa Sabato ya kweli ambayo tunapata kwa njia ya Yesu Kristo.

Kuna watu wengi kote ulimwenguni ambao hushika sana sheria ya Sabato. Wao huamini kwamba kumwabudu Mungu siku ya Jumamosi ni jambo ambalo Mungu mwenyewe ameamuru. Lakini jambo la majonzi ni kwamba kwa kufanya hivyo wao hukosa kuelewa kiini cha Sabato ya kweli. Kuna vikundi vingi vya kidini ambavyo washirika wake hutenda dhambi na kuishi dhambini na kukosa kutii Neno la Mungu, lakini wao hutuliza mioyo yao kwa kudumisha Sabato. Lakini ukweli wa mambo ni kwamba sisi hatumo sasa katika kipindi cha Agano la Kale na kiwango chetu cha utakatifu na pumziko tunalopata ni kikuu zaidi. Hiki ni kiwango ambacho hakikuwahi kupatikana kupitia kwa amri ya kupumzisha mwili na kufanya ibada katika siku ya Sabato.

Kuna somo ambalo linaweza kupatikana kwa kutazama wale ambao wangali wanadumisha Sabato hadi sasa. Kuna mambo ambayo yana mgongano tunapotafakari kuhusu vikundi vya Makanisa ya Siku ya Saba ambao hudai kwamba wao hudumisha sheria ya Mungu. Hii ni kwa sababu Agano la Kale hufundisha kuhusu utoaji wa kafara na uchomaji wa ubani, pia Agano hilo linafundisha kuhusu siku za kufanya sherehe kwa Bwana. Basi mgongano huo ni upi? Kuhusiana na Sabato Agano la Kale linafundisha kwamba wana wa Israeli hawakutakiwa kutoka "mahali" pao katika siku ya Sabato. Pia limetoa amri kwamba wale wote wanaofanya kazi katika siku ya Sabato wauawe. Je, waumini wa Siku ya Saba wanafuata mambo hayo? Basi ni jambo muhimu kwetu tusiwe watu wa kuchagua kile ambacho tutadumisha na kufundisha kutoka Agano la Kale. Hata ingawa kuna mengi ambayo tunajifundisha kutokana na Agano la Kale, tunao ujuzi wa kiroho ambao ni bora zaidi na ambao unamletea mtu toshelezo zaidi kupitia kwa Agano Jipya.

Lakini hata ingawa katika kipindi hiki tunachoishi tuna uhuru wa kufanya kazi na pia uhuru wa kuabudu adui wa maisha yetu ameingia katika swala hili. Waumini wengi huwa na shughuli nyingi hivi kwamba wao hukosa kufanya ibada ya pamoja ya ushirika wa watu wa Mungu kuwa ni jambo muhimu maishani mwao. Basi wao hufanya swala la kuhudhuria kanisa kuwa jambo la "kufanya au kutofanya" kulingana na shughuli zao za siku ya Jumapili. Basi ni jambo muhimu sisi tusisahau masomo makuu ambayo huwa na usaidizi kwetu kuhusu haja ya kupumzika na kumwabudu Mungu na ambalo ndilo jambo kuu linalofundishwa katika Agano la Kale.

Zaidi ya hayo hebu tufanye juu chini ili tuweze kuingia katika pumziko la kweli la roho zetu ambalo hupatikana ndani ya Kristo pekee wakati tunajitolea na kunyenyekea ili kupata usalama katika utakatifu wa Mungu.

*Michael W. Smith*

*Aprili 2017*

mengi kwa
MTANDAO

*Tutembelee kwa*

*www.thegospeltruth.org*

*ili uagize na kusoma*

*jarida letu.*

# MWONGOZO WA KUJIFUNZA BIBLIA: SABATO

**Somo la Biblia**: *Basi, mtu asiwahukumu ninyi katika vyakula au vinywaji, au kwa sababu ya sikukuu au mwandamo wa mwezi, au sabato; mambo hayo ni kivuli cha mambo yajayo; bali mwili ni wa Kristo.* — Wakolosai 2:16-17

**Muhstasari:** Udumishaji wa Sabato ni jambo ambalo liliamuriwa katika Agano la Kale. Sherehe hii ya kudumisha siku moja iliyotengwa na ambayo ni takatifu kwa Mungu ilitimia katika Agano Jipya kupitia kwa Yesu Kristo. Yeye ndiye ambaye hutoa pumziko la kweli kwa roho ya mwanadamu na mtoto wa Mungu anatakiwa kudumisha kila siku kama siku takatifu kwa Bwana.

**I. Kuanzishwa kwa Sabato na Sheria ya Musa**

- A. Kutoka 16:22-30 Sabato yasherehekewa kwa mara ya kwanza.
- B. Kutoka 20:8-11 Sheria yatolewa katika Mlima Sinai.

**II. Sabato Haikusherehekewa Kabla ya Wakati wa Musa**

- A. Nehemia 9:14 Ilijulikana kupitia kwa Musa.
- B. Kumbukumbu la Torati 5:15 Amri ya kuisherehekea ilitolewa baada ya ukombozi wa kutoka Misri.

**III. Sababu ya Kuanzishwa kwa Sabato**

- A. Kutoka 23:12 Pumziko.
- B. Kutoka 20:11 Kukumbuka Muumbaji/kazi ya uumbaji.
- C. Kumbukumbu la Torati 5:12-15 Kumbuka ukombozi kutoka Misri.
- D. Walawi 23:3-8; (19:30) Huu ni wakati wa ibada.

**IV. Sheria za Kuhifadhi Sabato**

- A. Kutoka 13:12-17 (35:2-3) Ilibidi yeyote aliyefanya kazi siku hiyo kuuawa.
- B. Hesabu 15:32-36 Mwanaume mmoja auawa kwa kupigwa mawe kwa kukusanya kuni siku ya sabato.
- C. Nehemia 13:17-19 Yuda yanajisi Sabato.

**V. Sheria ilikuwa Ndiyo Agano ya Wayahudi**

- A. Kutoka 31:17 Ishara kati ya Mungu na wana wa Israeli.

**VI. Agano la Kale Halifanyi Kazi Tena (tazama toleo la 18)**

- A. Waebrania 8:8-9, 13 Sheria ya Musa haifanyi kazi tena (Yeremia 31:31-32)
- B. Luka 16:16 Sheria ilikuweko hadi wakati wa Yohana Mbatizaji.
- C. Wagalatia 3:11-13 Hakuna mtu anayehesabiwa haki kupitia kwa sheria.
- D. Warumi 6:14 Hatumo tena chini ya sheria (Warumi 7:6).
- E. Matendo 15:5, 24, 28-29 Hakuna amri inayomuarisha Mkristo kudumisha sheria ya Musa.

**VII. Yesu na Sabato**

- A. Mathayo 12:1-8 Yesu asema mtu avunjaye masuke ili ayale hana makosa.
- B. Marko 2:27 Yesu ni Bwana wa Sabato.
- C. Mathayo 12:9-14 Ni jambo linalofaa mtu kutenda mema siku ya Sabato (Yohana 5:8, 9).

**VIII. Sabato ya Mkristo**

- A. Waebrania 10:1 Sheria ilikuwa kivuli cha mambo mema ambayo yangekuja.
- B. Mathayo 5:17 Yesu aitimiza sheria.
- C. Isaya 11:10 Pumziko lenye utukufu ambalo lilitabiriwa.
- D. Waebrania 4:1-11 Pumziko la kweli linapatikana kupitia kwa Kristo.
- E. Mathayo 11:28 Mungu ndiye anayepeana pumziko la kiroho.
- F. Wakolosai 2:16-17 Hakuna mtu anayestahili kumhukumu mwenzake kwa misingi ya siku takatifu au siku za sabato.
- G. Luka 1:74-75 Kila siku ni takatifu.

**IX. Siku ya Bwana: Ndio Siku ya Kihistoria ya Kufanyiwa Ibada za Kikristo.**

- A. Ufunuo 1:10 Siku ya Bwana.
- B. Luka 24:1 (Mathayo 28:1) Kufufuka kwa Yesu kulifanyika katika siku ya kwanza ya wiki.
- C. Matendo 2:1 Siku ya Pentekoste ilikuwa ni Jumapili.
- D. 1 Wakorintho 16:1-2 (Matendo 20:7) Wafuasi wa Yesu waliabudu siku ya Jumapili.


**Tamati:** *Bali sasa mkiisha kumjua Mungu, au zaidi kujulikana na Mungu, kwa nini kuyarejea tena mafundisho ya kwanza yaliyo manyonge, yenye upungufu, ambayo mnataka kuyatumikia tena? Mnashika siku, na miezi, na nyakati, na miaka.*

—Wagalatia 4:9-10



# Sabato

"Ikumbuke siku ya Sabato uitakase" (Kutoka 20:8). Amri ya nne ilianzishwa na Mungu wakati alipeana Amri Kumi hapo katika Mlima Sinai. Amri hiyo iliitenga Jumamosi, ambayo ni siku ya kwanza ya wiki, kuwa siku takatifu ya kufanya ibada katika Agano la Kale. Watu wa Mungu walitakiwa kufanya kazi siku sita lakini ya saba iwekwe wakfu kwa Mungu ili iwe siku ya pumziko ambako kazi yoyote haingefanywa.



Hata ingawa Mungu alipumzika katika siku ya saba baada ya kuumba ulimwengu . . . siku hiyo haikutakaswa hadi hapo baadaye.

## Mwanzo wa Sabato

Mara ya kwanza ambako kunanukuliwa Sabato kama siku ya mapumziko ni wakati ambapo Mungu alituma mana ili kulisha wana wa Israeli hapo jangwani baada ya wao kutoka Misri. Watu hao walikusanya mikate mara mbili kila ijumaa kwa sababu Mungu hakuwatumia mana siku ya Jumamosi kwa sababu ya "starehe takatifu (maanake) Sabato takatifu kwa Bwana" (Kutoka 16:22-30). Sherehe hii ilitiliwa nguvu na mkataba wa Mungu wa Amri Kumi ambako Yeye aliibariki sabato na kuifanya kuwa takatifu (Kutoka 20:11).

## Haikusherehekewa Kabla ya Wakati wa Musa

Hakuna rekodi au historia ya mababu wa wana wa Israeli wakisherehekea Sabato kabla ya sheria ya Musa kutolewa. Kulikuwa na miaka 2500 ya historia kabla ya nyakati za Musa ambako hakuna ushahidi dhabiti ya Sabato kusherehekewa kwa njia ya kanuni fulani. Nuhu na Ibrahimu waliishi kwa imani na wakapata neema machoni pa Mungu bila kuzingatia Jumamosi kama siku takatifu. Hata ingawa Mungu alipumzika katika siku ya saba baada ya Yeye kuumba ulimwengu (Mwanzo 2:3) siku hiyo haikutakaswa hadi hapo baadaye. Wana wa Israeli walijulishwa kuhusu Sabato takatifu "kwa mkono wa . . . Musa" (Nehemia 9:14) na amri kuhusu Sabato ikatolewa baada ya wana wa Israeli kukombolewa kutoka nchi ya Misri (Kumbukumbu 5:12-15).

## Kusudi la Sabato

Sabato au siku ya mapumziko ni siku ambayo ilianzishwa na Mungu katika Agano la Kale kwa kusudi na sababu tofauti tofauti. Ilikuwa ni siku ya mapumziko kwa watu na wanyama. "Siku sita utafanya kazi yako, na siku ya saba utapumzika; ili kwamba ng'ombe wako na punda wako wapate kupumzika, kisha mwana wa mjakazi wako na mgeni wapate kuburudika" (Kutoka 23:12). Hii hasa ilikuwa ni siku ya kukumbuka muumbaji wa ulimwengu (Kutoka 20:11); pia ilikuwa ni siku ya ukumbusho kwa wana wa Israeli ili neno litimie "utakumbuka ya kuwa wewe ulikuwa mtumwa katika nchi ya Misri, na ya kuwa Bwana, Mungu wako, alikutoa huko . . ." (Kumbukumbu 5:15). Basi siku ya Sabato ilikuwa ni siku iliyotengwa ili wana wa Israeli kuweza kuabudu kwenye masinagogi. Katika siku hiyo ambayo hakuna kazi ingefanywa, kulitakiwa kuwe na "makusanyiko matakatifu" ili kufanywe ibada kwake Bwana (Walawi 23:3-8).

## Sheria Iliyoandikwa

Wakati Mungu alisema Sabato idumishwe na Wayahudi Yeye hakuwa anatoa tu maoni bali alikuwa anatoa amri ambayo ilikuwa dhahiri na yenye manufaa; ndiposa amri iliyoandikwa ya kuandamana na Sabato ilikuwa yenye ukali mwingi. Ilikuwa kwamba Sabato haikuwa budi kudumishwa kama siku takatifu na "kila mtu atakayeitia unajisi hakika yake atauawa; . . . kila mtu atakayefanya kazi yo yote katika siku ya Sabato, hakika yake atauawa" (Kutoka 31:14-15). Kwa upande mmoja adhabu hii kali ilitolewa na Mungu kwa sababu wana wa Israeli walikuwa na kazi ya kujenga hema. Mungu hakutaka watu hawa washughulike sana kujenga hema hiyo hivi kwamba wakose kudumisha Sabato. Wana wa Israeli walikatazwa hata kuwasha moto kwa ajili ya kupika (Kutoka 35:2-3). Lakini Wayahudi walijua kwamba wangeweza kudumisha moto kwa ajili ya kutoa mwangaza na kupatia mwili joto.

Wakati wana wa Israeli walipokuwa jangwana walimpata mmoja wao akikusanya vijiti siku ya Sabato. Mtu huyo aliletwa mbele ya Musa na Aroni. Mungu naye akamwambia Musa kwamba mtu huyo alistahili kupigwa mawe hadi kufa hapo nje ya kambi, na mambo yakawa hivyo (Hesabu 15:32-36). Dhambi yake haikutokana na kutokujua lakini yeye alikuwa akivunja sheria ya Mungu kwa njia ya wazi, na alifanya hivyo huku akijua anavunja sheria ya Mungu. Ndiposa ukali wa Mungu ukaonekana kwa njia dhahiri.


## Sabato Inanajisiwa

Katika miaka ya baadaye watu wa nyumba ya kifalme ya huko Yuda waliinajisi siku ya Sabato. Milango ya mji huo ikafunguliwa kwa ajili ya usafiri na biashara (Nehemia 13:17-19). Lakini Nehemia akajaribu kufunga malango huku akjaribu kukatisha biashara kufanywa katika siku ya Sabato. Wafanyi biashara hao nao wakaweka vibanda nje ya kuta za miji huo hadi wakati gavana huyo alipokomesha jambo hilo kwa ajili ya kutakasa siku ya Sabato tena. Wakati watu waliacha kudumisha Sabato wao waliacha pia kumwabudu Mungu na ndiposa uovu

*(Inaendalea kutoka ukurasa 6)*

*(Endelea kutoka ukurasa 5)*

ukakidhiri. Kusema kweli kufanya kazi ili mtu apata mapato ya kidunia ni jambo lililokatazwa katika siku hiyo takatifu katika siku za ufuataji wa sheria. Lakini roho ya Sabato haikuwa ya utumwa bali ilikuwa ya furaha, roho ya kufanywa upya, ya rehema, ya kumbukumbu, na ya kufanya ibada.



## Ilitumika katika Nyakati za Agano la Kale

Sheria ya Sabato ilifanya kazi yake hadi hapo ambapo agano hilo lilipobadilishwa kwa njia mpya ya kuishi, njia yenye uhai. Kama ambavyo imetabiriwa katika Yeremia 31:31-32 na kukaririwa katika Waebrania 8:8-9, 13: "Maana, awalaumupo, asema angalia, siku zinakuja, asema Bwana, nami nitawatimizia nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda agano jipya; Halitakuwa kama agano lile nililoagana na baba zao, . . . Kwa kule kusema, Agano jipya, amelifanya lile la kwanza kuwa kuukuu. Lakini kitu kianzacho kuwa kikuukuu na kuchakaa ki karibu na kutoweka."

Kristo ndiye Sabato yetu na pumziko lake linashinda kwa ukubwa siku ile ya ibada ya kimwili ya kufanyika siku moja kwa wiki.

## Kristo Alileta Pumziko la Nafsi Zetu

Wakati Yesu Kristo alipokuja sheria ya Agano la kale haikuwa itumike tena: "Kwa kuwa torati ilitolewa kwa mkono wa Musa; neema na kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristo" (Yohana 1:17). Watu sasa hawakuwa utumwani wa sheria bali walikuwa kwenye uhuru wa roho, "Kwa sababu hamwi chini ya sheria, bali chini ya neema" (Warumi 6:14). Katika Agano la Kale Wayahudi walihesabiwa haki kulingana na jinsi walivyokuwa waaminifu kwa tamaduni na sherehe zao za kimwili. Lakini kwenye kipindi cha Agano Jipya mtu anahesabiwa haki kupitia kwa neema na imani ya Yesu Kristo: "Kwa maana wale wote walio wa matendo ya sheria, wako chini ya laana; . . . Ni dhahiri ya kwamba hakuna mtu ahesabiwaye haki mbele za Mungu katika sheria; . . . Kristo alitukomboa katika laana ya torati, . . ." (Wagalatia 3:10-13). Udumishaji wa Sabato ni jambo ambalo halijarudiwa katika Agano Jipya (Matendo 15:5, 24-29) na watoto wa Mungu wako huru kutokana na utumwa huo.

## Kristo Hakutilia Mkazo Swala la Sabato

Katika mafundisho yote ya Kristo Yeye hakutilia mkazo sheria ya Sabato, hata wakati akitilia mkazo baadhi ya amri zingine (Mariko 10:19). Yeye mwenyewe alilaumiwa na Mafarisayo kwa kuruhusu wanafunzi wake kuvunja masuke na kula (Mathayo 12:1). Yesu pia aliwaponya watu siku ya Sabato na kusema ni jambo linalofaa watu kutenda mema siku ya Sabato (Mathayo 12:9-14). Pia Yeye alimwamuru mtu aliyekuwa mngonjwa kuchukua mkeka wake na kutembea katika siku ya Sabato (Yohana 5:8-11). Lakini Yesu pia alishughulikia swala hili kwa kusema: "Akawaambia, Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya sabato." (Mariko 2:27). Kristo, kama mpatanishi na Mwana wa Mungu alikuwa na mamlaka ya kugeuza na kubadilisha mambo yaliyotakiwa kufanyika katika siku hiyo ya Sabato.

## Kuendelea Kushika Agano la Kale

Watu wengi wanaendelea kushikilia mafundisho ya Sabato kuwa yenye umuhimu mwingi hadi leo. Lakini maandiko yanafundisha kwamba watu wa Mungu hawako tena chini ya sheria. "Bali sasa mkiisha kumjua Mungu, au zaidi kujulikana na Mungu, kwa nini kuyarejea tena mafundisho ya kwanza yaliyo manyonge, yenye upungufu, ambayo mnataka kuyatumikia tena mnashika siku, na miezi, na nyakati, na miaka." (Wagalatia 4:9-10). Neno la Mungu pia linafundisha kwamba hakuna mtu anayestahili kumhukumu mwenzake "katika vyakula au vinywaji, au kwa sababu ya sikukuu au mwandamo wa mwezi, au sabato; mambo hayo ni kivuli cha mambo yajayo; bali mwili ni wa Kristo" (Wakolosai 2:16-17).

## Kristo Ndiye Sabato Yetu

Udumishaji wa Sabato haukuwa swala la tabia nzuri bali lilihusiana na swala la kisherehe. Katika Agano jipya sadaka, tamaduni, uchomaji wa ubani, ibada za hekalu, n.k. zimepita wakati wake kwa maana zimetimizwa na Yesu Kristo. Udumishaji wa Sabato ya kawaida kama siku takatifu ya mapumziko ilikuwa ni mfano wa pumziko la ajabu la kiroho ambalo linapatikana katika Yesu Kristo. Kristo ndiye Sabato yetu na pumziko lake linashinda kwa ukubwa siku ile ya ibada ya kimwili ya kufanyika siku moja kwa wiki. Waebrania 4:1-11 inashiriki kwa njia ya ajabu ukweli kuhusu pumziko la kweli la watu wa Mungu ambao huacha juhudi zao za kimwili na kuhesabiwa haki mbele zake Mungu na kuweza kuingia katika pumziko la Mungu kupitia kwa imani. Swala la udumishaji wa Sabato (ya kawaida) lilikuwa ni kivuli tu cha pumziko lenye utukufu, lisiloisha, na la kiroho ambalo linapatikana katika kipindi hiki cha neema; ndiposa Kristo anawaaliwaka watu wote kwa kusema: "Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha" (Mathayo 11:28).

## Pumziko la Kweli la Roho ya Mwanadamu

Udumishaji (kwa njia ya kimwili) wa siku takatifu ya kumwabudu Mungu ulikoma na badala yake kukaingia uwezo na nguvu kupitia kwa Kristo wa kuishi maisha matakatifu kila siku. "Ya kwamba atatujalia sisi, tuokoke mikononi mwa adui zetu, na kumwabudu pasipo hofu kwa utakatifu na kwa haki mbele zake siku zetu zote" (Luka 1:74-75).

Sabato ya kweli ya Mkristo katika kipindi cha Agano Jipya ni jambo lenye amani, pumziko, ibada za kiroho, na kuishi kwa utakatifu katika kila siku ya wiki. Kila siku ni takatifu na imetengwa kwa ajili ya ibada na ukumbusho wa ukombozi wa kutoka dhambini kupitia kwa Yesu Kristo. Tunamshukuru Mungu kwa ajili ya ujuzi huu wa Sabato ya ajabu!

—mws

# MASWALI na MAJIBU

## Je, ni kwa nini maandiko yanasema Sabato inastahili kudumishwa na vizazi vyote?

**Jibu:** Kutoka 31:16-17 inasema, “Kwa ajili ya hayo wana wa Israeli wataishika Sabato, kuiangalia sana hiyo Sabato katika vizazi vyao vyote, ni agano la milele. Ni ishara kati ya mimi na wana wa Israeli milele . . .”

Sheria ya Sabato ilikuwa ishara kati ya Mungu na taifa la Wayahudi. Sheria hiyo ilikuwa yao peke yao na ilikuwa ni moja kati ya sheria za taifa hilo. Sheria hii ilikuwa ya kudumu kama inavyodumu tohara kati ya Wayahudi, na pia kanuni kuhusu mkate wa kila wiki, ukuhani wa Walawi, n.k. Lakini kusema kwamba ni sheria ya kudumu sio kumaanisha kwamba ni sheria ya milele. Sheria ya Sabato (kama vile ambavyo sherehe zingine za Agano la Kale zilivyo) ilikuwa iwe ya kudumishwa kama sheria ya kutumika hadi hapo ambapo kungeundwa sheria nyingine kuchukua mahali pake. Mfano ambao unaashiriwa na sheria hiyo ulikuwa uendelee kudumu hadi hapo ambapo mfano mwingine mbadala ungeundwa mahali pake. Sabato ilitimizwa katika Kristo ambaye ndiye pumziko letu la Sabato, pumziko ambalo litadumu milele. Sheria ambayo iliwatenganisha Wayahudi kutoka kwa watu wa Mataifa iliondolewa kupitia kwa msalaba wa Kristo (Waefeso 2:11-18).

## Je, ni makosa mtu kufanya kazi siku ya Jumapili?

**Jibu:** Sisi hatuko tena chini ya sheria ya Sabato wakati ambapo ilikuwa haramu mtu kufanya kazi ya aina yoyote. Hata ingawa Wakristo kwa kawaida huabudu katika siku ya Jumapili kanuni za sheria ya Sabato hazikuingizwa katika siku ya Jumapili katika kipindi cha Agano Jipya.

Lakini hata tukishasema hayo tunahitaji kukumbuka kwamba “torati imekuwa kiongozi kutuleta kwa Kristo” (Wagalatia 3:24-25). Hata ingawa hatuko tena chini ya kiongozi huyo, silo jambo la busara mtu kusahau masomo yanayofundishwa na kiongozi huyo (maanake sheria). Moja ya sababu ya kuweko kwa Sabato ni kutoa kwa nafasi ili wanadamu (na hata wanyama) wapate siku ya kupumzika na ili waweze kuanza wiki mpya wakiwa na nguvu mpya kimwili na hata kiroho. Hata ingawa silo jambo la lazima kupumzika katika siku ya Jumapili, kunayo kanuni muhimu hapa ambayo ni ya msaada mkubwa. Kanuni hii ni kusema kwamba pumziko ni jambo linalohitajika na wanadamu, na watu huweza kufaulu vizuri zaidi katika fani mbali mbali ikiwa watakuwa na siku ambayo siyo ya kazi, na badala yake watilie mkazo swala la ibada na kutunza jamii zao.

Wakati mwingi watu wanatumia uhuru wao “(kuwa) sababu ya kuufuata mwili” (Wagalatia 5:13) na Jumapili inafanywa kuwa kama siku nyingine yeyote. Watu wanafanya kazi kupita kiasi na kujishughulisha na maswala ya maisha haya kwa kiwango cha kupita kiasi. Ndiyo sababu ibada ya Jumapili inakuwa jambo la kuharakishwa ili imalizike kwa haraka watu waondoke kwenda kazini mwao.

Lakini watu wa Mungu wanahitaji kutenga wakati wao wa kuwa na ibada pamoja na waumini wengine, na wasiruhusu shughuli za maisha haya kuingilia mambo muhimu zaidi. Hata ingawa sisi sio wadumishaji wa Sabato na hatustahili kuwa katika utumwa wa sheria, kunayo hekima na manufaa ya kiroho ya kuwa na siku maalum ya ibada, ambayo imetengwa na shughuli nyingi za maisha ya kawaida.

—mws

| Sabato ya Musa Ikilinganishwa na Sabato ya Mkristo | |
|---|---|
| Ni ya Kisherehe | Ni ya Kiroho |
| Inapumzisha mwili | Inapumzisha roho ya mtu. |
| Siku ya Saba idumishwe kuwa takatifu | Kila siku idumishwe kuwa takatifu. |
| Kazi za kimwili zilifanya siku hiyo kupoteza utakatifu wake. | Kufanya kazi au kutofanya hakuifanyi siku yoyote kuwa takatifu au kutokuwa takatifu. |
| Jitenge na kazi za kimwili. | Achana na kazi zote za dhambi. |
| Kufanya kazi siku ya Sabato kulileta hukumu ya kifo. | Kutenda dhambi huvunja pumziko la kiroho la Mkristo na humletea kifo cha kiroho. |
| Baraka za muda mfupi. | Baraka za kiroho |
| Mfano na Kivuli | Kutimia kwake |

JE, WAJUA?

### Mambo ambayo Yamenukuliwa kutoka kwa Wakristo wa Karne ya Pili

Sheria hii mpya inakutaka wewe kudumisha Sabato ya kila siku. Lakini je, wewe wadhani kwa sababu hufanyi kazi kwa siku moja tu jambo hilo linakufanya kuwa mtauwa . . . –Justin Martyr, 160 BK.

**Watakatifu hao wote ambao tayari wametajwa (Adamu, Habili, Henoko, Lutu, Melkizedeki) hawa ingawa hawakudumisha Sabato, wao walimpendeza Mungu.**
**–Justin Martyr, 160 BK**

Kama ambavyo tohara ya kimwili na sheria ya Kale ni mambo ambayo yamedhihirishwa kufika kikomo chako katika wakati fulani maalum, ndivyo ilivyo udumishaji wa Sabato ulivyoonyeshwa kuwa jambo la mpito. – Tertullian, 197 BK.

Neno Linalofaa kwa Msimu Huu

## Endelea Kudumu Ndani ya Bwana

*Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi, msipokaa ndani yangu.* —Yohana 15:4

Huduma iliyo na matunda mema huchukua muda na kumbidi mtu kujinyima mengi. Huduma hiyo inaweza kumchosha mtu sana kimwili na hata kihisia. Lakini baada ya huduma ya miaka mingi mhudumu yeyote mwenye kuelewa na aliye na uwezo wa kiakili anaweza kufanya mafafanuzi ya maandiko na kuweza kuonekana kana kwamba ana ukweli ndani yake. Hata ingawa kuna watu ambao wanaweza kujengeka kutokana na huduma kama hiyo, upako ule ambao huleta joto la ndani la huduma unaweza kuwa umekosekana ndani ya mhudumu huyo, na hivi kufanya huduma yake kuwa kazi ya hivi hivi tu, kuwa huduma ambayo ndani mwake haina uhai.



Huduma iliyo na manufaa haitokani tu na uwezo ambao mtu alizaliwa nao bali hutokana na tunda ambalo linakua ndani ya mhudumu kutokana na uhusiano wake wa kibinafsi na Yesu Kristo. Ndiposa Yesu akawashauri wanafunzi wake "Kukaa ndani yake" – kudumu pamoja naye, kuishi naye, kutembea naye. Kwa maneno mengine wao wadumu ndani yake.

Ni jambo linalohitajika na lililo na umuhimu kwamba wahudumu wake Bwana na hata watu wote wa Mungu wawe na uangalifu wakiwa kazini ya kuwahudumia watu wale wengine na wakati wanatimiza Wajibu Ule Mkuu ili wasikose kutilia maanani udumishaji wa uhusiano wao pamoja na Kristo. Adui yetu hutumia mambo yanayokubaliana na sheria na hata mambo yaliyo mema ili kuingilia kati katika mawasiliano yanayoleta umoja wa wahudumu pamoja na Roho ili kudhoofisha uhusiano kati ya watu wa Mungu na Mungu wao.

Wakati msukumo wa uchovu unaotokana na huduma unapogonga mwili wako kama mhudumu wa injili, tafadhali fanya bidii kumkaribia Mwenyezi Mungu. Hebu chukua wakati wako kumtafuta Bwana kibinafsi ili uweze kumkumbatia kwa ajili yako mwenyewe. Wakati kikombe chako kimejaa hapo ndipo utakuwa na uwezo wa kuwahudumia watu wale wengine kwa nguvu na kwa upako kutokana na uhusiano wako wa kibinafsi na Yesu Kristo. —mws

**Anwani**

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org